



Mamangu alipanda.

Alipanda bustani
ndogo.

Alipanda bustani
ndogo ya mbaazi.



Babangu alipanda.

Alipanda bustani
ndogo.

Alipanda bustani
ndogo ya maua.



Mamangu alipalilia
bustani zote mbili.



Babangu alinyunyizia
bustani zote mbili.



Mimi na wazazi wangu
tulifanya kazi katika
bustani hizo ndogo.

Mimi na dadangu
tulichuma maua na
kuvuna mbaazi.



Tulivuna magunia ya
mbaazi kutoka bustani
ndogo ya mbaazi.

Tulichuma magunia ya
maua kutoka bustani
ndogo ya maua.

Mamangu alipanda. Alipanda bustani kubwa. Bustani kubwa aliyopanda ilikuwa ya mbaazi. Babangu alipanda. Alipanda bustani kubwa. Bustani kubwa aliyopanda ilikuwa ya maua.



